

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI NA HALMASHAURI YA WILAYA MTWARA**



**MAANDALIZI YA MPANGO KABAMBE WA MTWARA**

**2015-2035**

**Imeandaliwa na:**

**Idara ya Mipangomiji**

**Kitengo cha Maliasili, Ardhi na Mazingira**

## **MPANGO KABAMBE NI NINI**

Mpango kabambe ni dira yakuongoza ukuaji wa mji wa Mtwara; kiuchumi, kijamii na kimazingira. Ni mpango unaoainisha na kuelekeza matumizi mbalimbali ya ardhi, kwa kuzingatia ukuaji wa Mtwara na mahitaji ya wadau wake wote kwa mtazamo wa miaka 20 ijayo kutokana na ugunduzi wa gesi asilia utakaopelekea ukuwaji wa viwanda.

Mapendekezo ya Mpango mpya kuhusisha maeneo ya Halmashauri ya wilaya ambapo kuna kata tisa zimeongezeka, yamepitishwa katika vikao vya kudumu vya Halmashauri ya wilaya na Manispaa ya Mtwara Mikindani.

## **MPANGO KABAMBE (2008-2028)**

### **MAFANIKIO**

- Mpango umesaidia kwa kiasi kuufanya mji wa Mtwara kuwa kati ya miji isiyokuwa na makazi holela
- Mpango ulifanikiwa kutenga maeneo ya matumizi mbalimbali na kuondoa migongano ya matumizi ya ardhi.

### **MAPUNGUFU**

- Ukosefu wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo
- Uandaaji wa mpango huo ulikuwana ushirikishi mdogo wa wadau.
- Mpango ulikuwa na eneo dogo ambalo lisineweza kukidhi mahitaji makubwa.

## **UANDAaji WA MPANGO KABAMBE MPYA WA 2015-2035**

Mpango huu umeandaliwa na halmashauri mbili, ambapo unahusisha eneo lote la Manispaa ya Mtwara Mikindani na eneo la kata tisa za Halmashauri ya wilaya ya Mtwara.


## **MALENGO YA MPANGO KABAMBE 2015 - 2035**

- Kuhamasisha matumizi ya Ardhi yanayozingatia tabia ya ardhi
- Kukidhi mahitaji ya wakazi wa Mtwara kwa ajili ya maeneo ya makazi, shughuli za kiuchumi, viwanda, kiutalii, huduma za jamii na burudani.
- Kuhakikisha kwamba; matumizi ya Ardhi yanazingatia mahusiano sahihi.na kutunza rasilimali
- Kuzuia mlundikano wa watu na kupunguza msongamano katika mifumo ya usafirishaji na huduma nyingine za umma.
- Kurahisisha upatikanaji wa mifumo ya,majisafi, usafirishaji,majitaka na miundombinu mingineyo.
- Kuboresha afya ya jamii ,usalama ,na ustawi wa umma.

## **UMUHIMU WA KUWA NA MPANGO KABAMBE MPYA**

- Kuhuisha rasmu ya Mpango kabambe ulikuwa wa kipindi cha miaka 20 kuanzia 2008 kuishia mwaka 2028 ambao haukuidhinishwa kutokana na kasoro kadhaa.
- Mpango wa sasa umehusisha baadhi ya maeneo ya Mtwara vijijini na kuwezesha kuwa na eneo kubwa kwa ajili ya upangaji na kutatua changamoto ya awali ya kuwa na eneo dogo la mpango.
- Kutafuta suluhisho la ongezeko la watu na mahitaji ya mbalimbali ya Ardhi pamoja na viwanda, ongezeko ambalo halikutarajiwa.

## Ramani ya matumizi ya sasa



## MAENEO MUHIMU KWENYE MPANGO KABAMBE

### 1. Takwimu za Idadi ya watu

Eneo la mpango lina jumla ya watu 161,600 ambapo mpango unalenga kuhudumia watu 799,357 ifikapo 2035.

### 2. Uchumi na ajira

Viwanda, Biashara rasmi na zisizo rasmi, Kilimo cha mjini, Ufugaji Uvuvi, Madini na uchimbaji, Misitu. Utarii na Uhifadhi wa maeneo ya asili Ajira na kipato.

### **3. Matumizi ya Ardhi**

#### **Mapendekezwa**

Ukubwa wa Ardhi iliyopo katika mpango ni **hekali 94600**. Makazi yaliyopangwa na yasiopangwa, Biashara, Viwanda, Taasisi, Maeneo ya wazi, Usafiri na Usafirishaji, Kilimo, Maeneo oevu na Misitu

4. **Nyumba na maendeleo ya makazi:** Mahitaji ya nyumba na namna ya kutatua changamoto ya upungufu wa nyumba Mtwara. Uboreshaji nyumba na makazi kwa mujibu wa sera ya nyumba na makazi ya mwaka 2000.

### **5. Huduma za Jamii**

Huduma za Elimu, Huduma za Afya na Utawala.

### **6. Miundo Mbinu**

Maji, Maji taka, Taka ngumu na Maji ya visima virefu.

### **7. Nishati**

Umeme, Mkaa, Kuni, Umeme wa Jua na Gesi

### **8. Usafiri, Usafirishaji na Mawasiliano**

Barabara, Reli, Usafiri wa Anga, Posta, Intaneti, Radio na Televisheni

## **UTEKELEZAJI WA MPANGO**

Watekelezaji wa mpango huu ni Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara na Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ikisimamiwa na Ofisi ya katibu Tawala Mkoa pamoja na Wizara ya Ardhi Nyumba na Mendeleo ya Makazi. Pia wadu wa maendeleo watakuwa watekelezaji wa mpango huu.

Eneo la mpango limegawa katika kanda tano za kimipango miji ambapo kila ukanda unaelezewa kwa kuangalia matumizi makubwa yaliyopo. Kanda hizi ni; Kanda ya Naumbu ambayo ni ya Viwanda, Kanda Nanguruwe ambayo ni ya Afya, Kilimo, Viwanda vya Mazao ya kilimo na Michezo, Kanda ya Mjimwema ambayo ni ya Elimu, Kanda ya Ziwani ambayo ni ya usafiri na Usafirishaji pamoja na Ukanda wa mjini kati ambao ni wa biashara na ofisi za taasisi mbalimbali.

# Ramani ya Mapendekezo

